

# SALA YA MJA CHOCHOLE.

Anophrine D. Shirima,  
November, 2022,  
Mwanza.

$\text{♩} = 65$

1.Ee Mu u mba wa du ni a, wa tu na wa nya ma pi a,  
2.Tu ma i la nguKa ri ma, Ra bi mwe nye si fa nje ma,  
3.Pi ndi ni o na po khe ri, a ma ni o na po shwa ri,

5

Kwa ko ni na ki mbi li a, sa la ma ku ji pa ti a,  
Ndi ko na pa ta 'sa la ma', tu fa ni i ja po vu ma,  
Ja mbo mo ja ni dha hi ri, Ye ye ni Mu ngu ho da ri,

9

mo yo u lo' nyo n'go nye a, ti ba u pa te po ke a.  
Dhi ki zi ki ni sa ka ma, I ma ra ni ta si ma ma.  
Si to zi le ta je u ri, Dha ha ma zi ki sha mi ri.

## **SALA YA MJA CHOCHOLE**

1. Ee Muumba wa dunia, watu na wanyama pia,  
Kwako ninakimbilia, salama kujipatia,  
Moyo ulo'nyon'gonyea, tiba upate pokea.
2. Tumai langu Karima, Rabi mwenye sifa njema,  
Ndiko Napata ‘salama’, tufani ijapovuma,  
Dhiki zikinisakama, Imara nitasimama.
3. Pindi nionapo kheri, ama nionapo shari,  
Jambo moja ni dhahiri, Yeye ni Mungu hodari,  
Sitozileta jeuri, Dhahama zikishamiri.